

**MAELEZO YA MHE. KAPT (MST) GEORGE H. MKUCHIKA (MB), WAZIRI WA
NCHI OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA
BORA WAKATI WA HAFLA YA UZINDUZI WA JENGO LA OFISI YA
TAKUKURU WILAYA YA MANYONI - SINGIDA
SEPTEMBER 02, 2020**

**Mhe. Job Ndugai (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya
Muungano wa Tanzania;**

**Bibi Sabina Seja, Mkurugenzi wa Uzuiaji Rushwa wa
TAKUKURU na Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa
TAKUKURU;**

Mhe. Rahabu Magwisa, Mkuu wa Wilaya ya Manyoni;

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Wilaya;

Viongozi na Watumishi wa TAKUKURU;

Wageni Waalikwa;

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana; Habari za asubuhi.

Mheshimiwa Spika,

Kwa heshima kubwa, ninaungana na viongozi wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa baraka zake na kwa kutuwezesha kukutana leo hapa Wilayani Manyoni.

Vilevile, ninatumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi **Mhe. Spika** kwa kutekeleza agizo alilolitoa Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kukutaka utuzindulie jengo hili la Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Wilaya ya Manyoni - Singida. **TUNAKUSHUKURU SANA!**

Mheshimiwa Spika,

Ninapenda kutumia fursa hii kuungana na Mheshimiwa Rais kuipongeza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuzuia na kupambana na watu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa hapa nchini.

Sote tulimsikia Mheshimiwa *Dkt.* John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa akituzindulia jengo la TAKUKURU Wilaya ya Chamwino - akiwasifu sana watumishi TAKUKURU kwa namna walivyochapa kazi katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake.

Ni matumaini yangu kuwa sifa hizi zimewapa TAKUKURU ari na ujasiri zaidi wa kushughulikia kero ya rushwa nchini na kuhakikisha kuwa mnaendana na KASI YA UTENDAJI KAZI WA MHESHIMIWA RAIS NA WASAIDIZI WAKE. Kwa weledi na ujasiri mlionao sina shaka kwamba mtaendeleza mapambano haya na moto huu mliouwasha hautazimika kwa namna ye yote ile.

Mheshimiwa Spika,

Sifa alizozitoa Mheshimiwa Rais zinaendana na utendaji kazi wao. Kwa mfano katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Juni 2020 TAKUKURU Mkoa wa Singida wamefanikiwa kukamilisha uchunguzi wa majalada 28, pia wamefungua kesi mahakamani 36 na kufanikiwa kushinda kesi 10 na kushindwa kesi 4.

Aidha kiasi cha Tsh. **199,559,254/=** kiliokolewa kutokana na operesheni mbalimbali zilizofanyika kama ifuatavyo:-

- (i) Tsh. 58,150,000/= ziliokolewa kama mikopo umiza.
- (ii) Tsh. 85,329,500/= zilirudishwa kutoka kwa wanachama wa vyama vya ushirika.
- (iii) Tsh. 44,623,254/= mapato yaliyotokana na usimamizi wa madini.
- (iv) Tsh. 11,456,500/= mapato yaliyotokana na usimamizi wa minada.

Pia katika kipindi hicho hicho TAKUKURU Mkoa wa Singida walifanikiwa kufungua na kuimarisha klabu za Wapinga Rushwa mashuleni na vyuoni 234 na kutoa semina na mikutano ya hadhara 225. **Hongereni sana!**

Mheshimiwa Spika,

Ninafahamu kwamba jukumu lililonisimamisha hapa ni kuzungumza maneno machache ya kukukaribisha, hivyo baada ya kusema hayo machache, sasa kwa niaba ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) pamoja na hadhara yote iliyoko hapa, ninakukaribisha ili uzungumze nasi na hatimaye utuzindulie jengo hili la Ofisi ya TAKUKURU WILAYA YA MANYONI mkoani Singida.

Mheshimiwa Spika, KARIBU.